

**BODI YA USAJILI WA WABUNIFU MAJENGO NA WAKADIRIAJI MAJENZI**  
**(Chini ya Sheria Na. 4 ya Mwaka 2010)**



**Tangazo la nafasi za kazi ya Udereva**

**Utangulizi:**

Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi ni taasisi ya serikali ambayo imeanzishwa kwa sheria Na. 4 ya mwaka 2010. Mojawapo ya majukumu yake ni kusajili na kuratibu Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi na Wataalamu wanaoshabihiana nao.

Bodi inakaribisha maombi ya kazi ya Udereva Daraja II kwa mkataba katika Ofisi zake zilizoko **Dar es Salaam, Mbeya na Dodoma.**

**Sifa za Muombaji:**

Muombaji anatakiwa kuwa na cheti cha kuhitimu kidato cha nne (Certificate of Secondary Education), leseni ya udereva daraja "C" na uzoefu wa kuendesha magari kwa muda usiopungua miaka mitatu bila kusabisha ajali. Sambamba na hilo Muombaji anatakiwa kuwa na cheti cha majarabio ya ufundi wa magari, daraja la III kutoka VETA pamoja na cheti cha udereva mahiri daraja la pili kutoka Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT).

**Majukumu ya Kazi:**

- Kuendesha gari la Taasisi.
- Kutunza na kuandika daftari la safari (log- book) kwa safari zote.
- Kufanya uchunguzi wa gari kabla ya safari ili kugundua ubovu unaohitaji matengenezo.
- Kufanya matengenezo madogo madogo ya gari.
- Kuhakikisha gari na vyombo vyake vipo katika hali nzuri wakati wote.
- Kutekeleza kazi nyingine yoyote atakayopangiwa na mkuu wake wa kazi.

**Mshahara:**

Kwa kuzingatia viwango vya mishahara ya Bodi.

Nafasi : Tatu (3)

**Masharti kwa Muombaji:**

- Muombaji awe raia wa Tanzania.
- Barua ziambanishwe na vyeti husika ambavyo vimethibitishwa na mwanasheria na maelezo binafsi ya muombaji (CV) yaliyosainiwa.
- Barua ziwe na anwani na namba za simu za kuaminika.
- Majina, anwani na simu za wadhamini wawili wanaomtambua muombaji.

Maombi yatumwe kwa anwani ifuatayo kabla ya tarehe **20 Novemba 2018.**

**Kaimu Msajili,**  
**Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi,**  
**S. L. P. 72673, Simu: 2110292, Jengo la Tetex, Ghorofa ya pili, DAR ES SALAAM.**  
**Barua Pepe: [info@aqrb.go.tz](mailto:info@aqrb.go.tz) Tovuti: [www.aqrb.go.tz](http://www.aqrb.go.tz)**